# 2017
# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KARATASI YA KWANZA 102/1- INSHA KIDATO CHA 3

**1. Insha ya lazima**

Shule Fulani katika kaunti yenu imetangaza nafasi ya kazi kwa mwalimu wa Kiswahili.
.Umealikwa kushiriki mahojiano. Andika tawasifu utakayowasilisha kwa jopo tathmini.

**Insha iwe na sifa zifwatazo**

a) Kichwa

Kichwa kionyeshe ni tawasifu ya nani.
Maelezo mengi yasitolewe ila kubaini tu kuwa ni tawasifu yako.
KIELELEZO:TAWASIFU YANGU

b) Utangulizi:

- ✓ Hapa mtahiniwa amjengee msomaji usuli wake hasa.
- ✓ Mtahiniwa aeleze usuli wake:tarehe,siku na mahali alikozaliwa.
- ✓ Mtahiniwa anaweza kuyaangazia maswala ya uzawa wake,yaani mahali ambako alizaliwa,pengine yeye ni mwana wa ngapi katika familia hiyo.
- ✓ Anaweza kusema yeye ni mtoto wa nani kwa kutaja majina ya wazazi wake.
- ✓ Anaweza pia kumchorea msomaji umbo na sura yake.
- ✓ Hali ya kiuchumi alimozaliwa:Kipengele hiki kitakuwa muhimu kwani kitaonyesha uhitaji wake na namna ambavyo aliweza kuhimili hali hii ya uchechefu na kufaulu.

c) Mwili

Mtahiniwa aangazie:

(i) Safari ya kisomo cha msingi

- ✓ Aangazie masomo yake katika daraja la chini zaidi la masomo-shule ya msingi.
- ✓ Alisomea wapi?Vipindi vipi?Ni matukio yapi ya kukumbukika yaliyomwathiri sana katika wakati wake alipokuwa akiendelea na masomo?

(ii) Safari ya ShuleYaUpili

Alisomea wapi ?Kwa kipindi kipi?
Alikuwaje shuleni kimasomo pamoja na katika nyanja nyingine kama vile michezo na maswala ya vyama.
Alishikilia vyeo vipi katika uongozi.
Ufanisi wake katika masomo na fani nyingine.

(iii) Safari ya Masomo Ya Juu

Alisomea chuo kipi?
Alisomea huko katika kipindi kipi na shahada hii ilikuwa katika taaluma ipi?
Maswala mengine chuoni yaangaziwe:Uanachama katika vyama tofauti pamoja na majukumu aliyoyatekeleza.
Muhimu: Mtahiniwa ni sharti atoe maelezo yanayoegemea **ualimu** kwa vile ndicho kiini kikuu cha swali.

(iv) Tajriba Ya Kikazi:

Aonyeshe ni mashirika yapi ya habari amepata kufanyia kazi.
Aonyeshe nyadhifa ambazo amewahi kushikilia katika mashirika hayo.
Aonyeshe amefanya nini katika harakati zake za kujiimarisha kitaaluma:ameshiriki makongamano au warsha zozote?
Katika kipindi chake cha kazi akiwa ameshikilia nyadhifa mbalimbali,mashirika hayo yalipata ufanisi na kuimarika kwa njia gani?
Je,amepata matuzo yapi kutokana na utendakazi wake mzuri?

d) Hitimisho

Katika kuhitimisha,mtahiniwa ajitanue kwa kuonyesha upekee wake.
Aonyeshe kuwa ana mbinu na uwezo wa kufanya kazi.
Aahidi kuwa kazi yake itakuwa aula.
Ashukuru jopo tathmini kwa kumpa nafasi ya kushiriki mahojiano.

**Tanbihi;**

Sifa zote za tawasifu zidhihirike katika insha ya mtahiniwa,vinginevyo atakuwa ameboronga mtindo.Akadiriwe vilivyo.

Mtahiniwa atumie nafsi ya kwanza katika kuandika.Atakayetumia nafsi tofauti atakuwa amepotoka.Atuzwe D 03/2

2. Teknolojia ya kisasa ina manufaa vilevile ina madhara si haba. Jadili.

Ni swala la mjadala. Kuna hoja za kuunga na hoja za kupinga. Mwanafuzi atoe uamuzi mwishoni kulingana na uzito wa hoja zake.

Tazama upande ambao ameegemea. Huo ndio msimamo wake. Hoja zozote tano zinafaa.

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:

Maji ya mbali hayamalizi kiu.

Hii ni insha ya methali. Mwanafunzi ashugulikie sehemu zote mbili za methali katika kisa atakachobuni. Kisa kibainishe kinyume cha matarajio kuhusu matendo ya wanaohusika.

4. Tungakisakitakachomalizikakwamanenoyafuatayo:

..hapo ndipo nilipogundua ya kwamba kila kilicho na mwanzo bila shaka hakikosi hatima yake.

(i) Mtahiniwa amalizie kwa maneno haya. Anayekosa kumalizia kwayo amejitungia swali na atuzwe D 01/20 au 02/20

(ii) Anayeongeza maneno chini ya matano, achukuliwe kuwa na kosa la mtindo na akadiriwe ifaavyo.

(iii) Anayekata au kusahau maneno chini ya matano achukuliwe kuwa na kosa la kimtindo;akadiriwe ifaavyo.

**Uhusika**

Asiyezingatia nafsi ya kwanza atuzwe D 01/20 au 02/20.